

“Maumivu 50 Wakati Dhoruba Linapoanguka Katika Hema La Ufufuo”

na

Ellis P. Forsman

“Maumivu 50 Wakati Dhoruba Linapoanguka Katika Hema La Ufufuo”

na

Ellis P. Forsman

Mei 1, 2013

“Maumivu 50 Wakati Dhoruba Linapoanguka Katika Hema La Ufufuo”

Nukuu iliyo hapo juu ilionekana katika toleo la habari AP, katika Telegramu Ya Nyota ya Ngome, Ngome Bora, Texas, tarehe ya Sept. 11, 1950. Tukio lilitokea Amarillo, Texas wakati Oral Robert alipofanya “Maji ya Uponyaji na Ufufuo”

Kipande cha taarifa:

“Hema la ufufuo lilianguka wakati wa upepo na mvua iliyojaa radi hapa jumapili jioni, ikijeruhi takribani watu 50. Katika saa za jioni hakukuwa na taarifa za vifo au watu waliojerehiwa sana miongoni wa watu 7,000 waliokuwepo kwenye mkutano wa Oral Robert wa huduma ya imani inayo okoa.”

“Mashahidi walisema upepo mkubwa uliingia chini ya hema lile wakatika wa mvua kubwa na dhoruba, likibeba hema \$ 22,000.00 na vyuma na kuliangusha kwa waumini. Zaidi ya nusu la kusanyiko lilizikwa kwenye uchafu na vumbi.”

“Wengi wa wale waliotibiwa katika hospitali za kawaida walikuwa na majeraha ya kukatwa, kuburuzwa, na wachache walioumia walivunjika. Magari yote ya wagonjwa yaliyokuwepo, madaktari, na manesi walikimbizwa katika tukio.”

Bwana, Robert “mponyaji” mkuu, aliyedai kwamba Mungu alimruhusu “kuwaponya” maelfu, hakuweza kufanya hata muujiza mdogo katika tukio hili. Upepo haukutii sauti yake! Hakuweza hata kuponya mikono na mbavu zilizovunjika! Hakuweza hata kuponya kidole kilichovunjika. Kwa nini, hakuweza hata kuponya jeraha dogo kwenye mkono, hata muujiza mdogo.

Kwa nini majeruhi waliwahisha hospitalini? Kwa nini waliojeruhiwa walitibiwa katika mahospitali ya kawaida? Kwa nini, “magari yote, madaktari, na manesi” waliwahisha katika “Hema lililo kunjwa kunjwa la Uponyaji? Robert alikuwa akifanya muujiza mbele ya watu 7,000, akidai kwamba ni “muujiza mkuu na uponyaji” uliyokuwa unafanyika. Huu ulikuwa ni wakati mwafaka kwake kujithibitisha. Angeweza kuwa na “waumini” wengi kwa kufanya muujiza mdogo baada au wakati wa tukio hili. Lakini, rafiki yangu, hii ilikuwa ni kitu halisi; hakuna uongo juu ya mbavu zilizoburuzwa na miguu iliyovunjika. Dhoruba la kati lililotokea Texas lilimuweka nje ya biashara ya “uponyaji” wakati uo huo. Alihama kutoka Amarillo, Texas, na kuwaacha madaktari na manesi ili “waponye” waliojeruhiwa katika hospitali.

Katika mwaka wa 1970 huko Seattle Washington, mwanamke mmoja ambaye mke wangu anamfahamu akatuambia kwamba amekuwa mgonjwa sana na kwamba alikuwa naenda katika hospitali ya Oral Robert ili aweze kuponywa. Aliporudi nyumbani, akatuambia kwamba hospitali imefanya vipimo ili kujua ugonjwa ulikuwa ni nini. Aliambiwa kwamba kilichokuwa kinamwuguza hakikua kibaya sana. Walimfanyia huduma ya uponyaji na wakamwambia kuwa ameshaponya na wakamruhusu kwenda

nyumbani. Ugonjwa wake ukawa mbaya sana, hivyo akaenda na kumwona daktari aliyemwambia kwamba ana kansa. Akaeleza, “Yawezaje kuwa hivyo, niliponywa katika hospitali ya Oral Robert.” Daktari akamwomba ampe vipimo alivyopimwa katika hospitali ya Oral Robert lakini vilikataliwa. Akapelekewa agizo la mahakama na kulazimisha hospitali hiyo ipeleke sitakabadhi zote. Katika risiti za takwimu daktari alikuta ni kwa nini hawakutaka kupeleka sitakabadhi zao; maandishi ya mkono yaliyoandikwa na Oral Robert yalisomeka “MSIMWAMBIE mgonjwa kwamba ana kansa; mmuruhusu kwenda nyumba na mwambieni kuwa ameponywa”. Mama huyu alikuwa amechanganyikiwa! Hakuwa na uwezo wa kwenda kulishitaki hospitali hii mahakamani; baadaye akafa siku chache zilizofuata.

Wengi wamedanganywa na uponyaji huu wa uongo na wengine kama yeye waliotengeneza mamilioni za dola katika “huduma” hii.

